


# TIRA
## BULLETIN

**YALIYOMO**

- **DKT. HUSSEIN MWINYI AWAPOKEA MABALOZI WA BIMA IKULU YA ZANZIBAR**
- **DKT. DOTTO BITEKO AKUTANA NA WADAU WA BIMA**
- **KATIBU MKUU KIONGOZI AWAPOKEA MABALOZI WA BIMA**



**WAHARIRI**

Hadija Maulid
Tabia Mchakama

**TIRA**

**KWA SOKO SALAMA LA BIMA**



## DKT. HUSSEIN MWINYI AWAPOKEA MABALOZI WA BIMA IKULU YA ZANZIBAR

Tarehe 4 Septemba, 2023 katika Ikulu ya Zanzibar, Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ametambulishwa rasmi Mabalozi wa Bima Tanzania ambapo amepongeza jitihada zinazofanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) katika kukuza soko la bima nchini.

Mhe. Rais, amesema Mabalozi wa Bima watasaidia kujenga uelewa wa maswala ya Bima kwa Viongozi mbalimbali Serikalini. Aidha Dkt. Mwinyi ameipongeza TIRA kwa kuunda Konsotia Mbili za Kilimo na Gesi ambapo zitasaidia Kuongezeka kwa upatikanaji wa mtaji katika ulipaji wa fidia na madai ya Bima kwenye sekta ya kilimo na gesi kwani itawawezesha kampuni za Bima Tanzania kuwa na mtaji mkubwa na hivyo kuepuka wananchi kukata Bima za aina hiyo nje ya Nchi kitendo kinachoikosesha Tanzania fedha nyingi.

Awali akitoa utambulisho wa Mabalozi hao, Dkt, Baghayo A. Saqware, Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania amewataja Mabalozi hao kuwa ni Mhandisi Zena Said, Katibu Mkuu Kiongozi SMZ na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Wanu Ameir, Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Japhet Hasunga, Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wakati akielezea taarifa ya Maendeleo ya sekta ya Bima Dkt. Saqware amesema, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wameanzisha Konsotia ya Bima ya Mafuta na Gesi ambapo Vihatarishi vyote vya nishati vinavyotoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama vile vihatarishi kutoka kwa mradi wa LNG vitakatiwa bima kupitia Konsotia ya bima ya nishati ya mafuta na gesi Tanzania. Kwa mantiki hiyo ,miradi yote ya gesi na mafuta itakuwa na uwezo wa kubakiza zaidi ya asilimia 45 ya ada zitokanazo na gesi na mafuta.

> “Nawapongeza kwa kupanua wigo na sasa mmeingia kwenye kilimo na gesi kwani Watanzania wengi wanajihusisha na kilimo, hivyo endeleeni kutoa elimu juu ya konsotia hizi ili kujenga Imani kwa wananchi na hatimaye pesa nyingi zibakie nchini”
>
> **Amesema Dk. Mwinyi**













# DKT. BITEKO AKUTANA NA WADAU WA BIMA

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko Septemba 19, 2023 amekutana na Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo A. Saqware pamoja na Naibu Kamishna Bi. Khadija I. Said ambao waliambatana na Mabalozi wa Bima, Viongozi wa TIRA Pamoja na Kamati ya Ufundi ya Konsotia ya Mafuta na Gesi wamekufanya mazungumzo yenye lengo la kutoa fursa kwa kampuni za Bima zilizosajiliwa nchini kushiriki katika uchumi wa mafuta na gesi.

Kamishna wa Bima amemueleza Dkt. Biteko kuwa Konsotia ya Bima iliyozinduliwa Novemba 2022 inaundwa na umoja wa kampuni 22 za Bima zenye mtaji wa jumla ya Dola za Kimarekani Mil. 6. Aidha kamishna ameeleza kuwa malengo ya Mamlaka na Konsotia kwa ujumla ni kuhakikisha miradi yote ya gesi na mafuta inabakiza sio chini ya 45% ya ada zinazotokana na mafuta.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Mhandisi Zena Said, amesema Sekta ya bima nchini imejidhatiti katika kuweka uwekezaji mkubwa ili kuvutia miradi mikubwa nchini na nje ya nchi na kukata bima kwenye kampuni za hapa nyumbani ili fedha hizo zibaki nchini na hatimae kukuza uchumi na kwamba serikali iziamini na kufanya biashara na kampuni hizo

Mhe. Naibu Waziri Mkuu ameuhakikishia ujumbe huo wa Sekta ya Bima kuwa Serikali inaamini katika kuwajengea uwezo wazawa ambao wanaonyesha uwezo katika maeneo mbalimbali ikiwemo hii sekta ya bima na kuwataka waendelee kuwa wabunifu katika biashara zao na kwamba Serikali ipo tayari kutoa ushirikiano stahiki.

Nao Mabalozi wa Bima Mh. Japhet Hasunga na Mh. Wanu Ameir kwa upande wao wamemshukuru Mh. Dkt. Biteko kwa kufungua Milango kwa kampuni za Kitanzania za Bima kutumia fursa zilizopo nchini na nchi Jirani ili kuimarisha biashara zao.

Kampuni zinazounda Konsotia ya Mafuta na Gesi ni 22 ambapo TanRE ni Msimamizi wa Konsotia huku Phoenix ikiwa ni Kampuni kiongozi.

# KATIBU MKUU KIONGOZI AWAPOKEA MABALOZI WA BIMA



Katibu Mkuu Kiongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Balozi, Dkt. Moses M. Kusiluka pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Mhandisi Zena A. Saidi wamefanya kikao cha siku moja na Viongozi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ambapo ametambulishwa rasmi na kuwapokea Mabalozi wa Bima na pia kujadili maendeleo ya sekta ya bima nchini.

Mabalozi wa Bima waliotambulishwa katika kikao hicho kilichofanyika Septemba 1, 2023 kwenye ukumbi wa Mikutano wa ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi Zanzibar ni Mhandisi Zena A. Said Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Japhet N. Hasunga Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Mhe. Wanu H. Ameir Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Mabalozi hao walioteuliwa Mwezi Februari 2023 majukumu yao ni Kutoa ushauri kwa Mamlaka na sekta ya bima kwa ujumla kuhusu maendeleo ya sekta ya bima na pia kutoa elimu kwa umma juu ya masuala ya bima katika ngazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi na Makatibu Wakuu kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar.

Balozi Dkt. Kusiluka pamoja na kukubali kuwa Balozi wa vitendo wa bima, amesema Makampuni ya bima yaongeze wigo wa bidhaa zao za bima na pia Mamlaka



kutoa elimu kuhusu vipengele mbalimbali vya bima ambazo Serikali, mashirika binafsi na mtu mmojammoja wanaweza kuzitumia. Amesema Serikali ina mpango wa kupanua wigo wa kuzikatia bima mali zake mbalimbali baada ya utafiti kufanyika juu ya aina na







na gharama za kukatia bima mali hizo.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Dkt. Juma M. Akili Katibu Mkuu Afisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar pamoja na Dkt. Natu E. Mwamba Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni watendaji wakuu katika wizara Mama ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania Katika maelezo yake ya Utangulizi Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Wawakilishi Mhandisi Zena A. Saidi amesema tangu kuchaguliwa kwa mabalozi Mwezi Februari 2023 tayari wamepata mafunzo kuhusu umuhimu wa bima ambapo imewajengea uwezo wa kutoa elimu kwa umma na kwa wabunge.

Mabalozi wamekuwa mstari wa mbele kuishauri Serikali kuhusu umuhimu wa ukatiaji bima wa mali za Serikali.

Akielezea mafanikio katika sekta ya bima Kamishna wa Bima Dkt. Baghayo A. Saqware amesema Mchango wa Sekta ya Bima kwenye pato la Taifa unazidi kuongezeka kutoka asilimia 0.56% kwa mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 1.68% kwa mwaka 2021.

Pia Mamlaka imeendelea kuongeza gawio Serikalini ambapo kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Juni 2023 Mamlaka imeweza kulipa gawio kwa Serikali la jumla ya Tsh. Bilioni 2.9

Kwa upande wa ajira Kamishna amesema sekta ya bima imechangia kwenye ajira kwa vijana ambapo hadi Septemba 2022 imetoa ajira za kudumu kwa Watanzania 4, 173 ukilinganisha na 3,208 kipindi kama hicho mwaka 2021.

Kikao hicho kilihitimishwa kwa azimio la kwamba Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania inasisitizwa kuendelea kutoa elimu kwa watu mbalimbali wakiwemo Makatibu Wakuu na Wabunge. Imeelekezwa semina ya Bima ifanyike kwa Makatibu Wakuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Makatibu wa Serikali ya Mapandizi ya Zanzibar.

Upande wa TIRA pia uliwakilishwa na Naibu Kamishna Bi Khadija Said, Meneja Ubora na Udhibiti wa Vihatarishi Bw. Zakaria Muyengi pamoja na Meneja Uhusiano na Mawasiliano Bi. Hadija Maulid.


























**TIRA**BULLETIN